# STANDARD OPERATING PROCEDURE PALLIATIVE CARE UNIT

1. Tunapokea wagonjwa wa rufaa iliyoandikwa na daktari toka klinic, wodini, (majumbani na hospitali nyingine).
2. Mgonjwa wa nyumbani awe na faili lenye usajiliwa wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na kuingizwa kwenye INAYA pia wagonjwa wapya wanasajiliwa na kitengo cha tiba shufaa na kuingizwa kwenye INAYA.
3. Rufaa itaelezea sababu ya mgonjwa kuletwa kwenye kitengo hiki.
4. Mgonjwa atafahamishwa sababu ya yeye kuwepo hapo na mategemeo yake baada ya kupewa huduma.
5. Wagonjwa wote pamoja na familia zao wataangaliwa kimwili, kijamii, kisaikologia, na kiroho.
6. Wagonjwa watapatiwa dawa na mahitaji mengine kutokana na hitaji la mgonjwa husika.
7. Wagonjwa wenye maumivu makali watapewa dawa kulingana na kiwango cha maumivu yao na dawa itaandika kwenye cheti maalumu cha dawa.
8. Wagonjwa ambao watahitaji dawa ambazo kwenye taasisi hakuna, watapewa cheti kwenda kununua kwenye maduka ya nje ya dawa.
9. Morphine solution itaandikwa na daktari au nurse ambaye aliyeenda mafunzo ( ya toka Diploma na kuendelea) na aliyeruhusiwa kuandika dawa hiyo na pamoja na dawa zingine za kuondoa maumivu.

10.Wagonjwa ambao wataanzishiwa dawa ya morphine watapewa kadi ya blue, ambayo atatakiwa kuja nayo kila anapokuja kuchukua dawa.

11.Wagonjwa wanaoanza dawa ya morphine kwa mara ya kwanza watapewa dawa ya siku saba(7) na kumuomba mgonjwa arudi kwa ajili ya kukagua au kutathimini maumivu.

12.Mgonjwa/ndugu wale ambao wanatoka mbali na wamekuja kwa ajili ya marudio atapata dawa ya wiki mbili(2) mpaka mwezi mmoja(1) kulingana na umbali anakotoka.

13.Kila mgonjwa anayetumia morphine lazima wapewe dawa ya kulainisha choo.

14.Wagonjwa na familia wenye matatizo mengine ya kijamii, kisakologia, kiroho watapewa rufaa kwenda vitengo vinavyohusika: mfano kwa - Social Worker, Msakologia, Mtoa ushauri nasaha na Viongozi wa dini(Spiritual leaders).

15.Mgonjwa /ndugu atakuwa na mawasiliano na timu ya tiba shufaa muda wowote.

16.Ndugu wa mgonjwa hasa wa mikoani wanaruhusiwa kuwachukulia dawa wagonjwa/mgonjwa wao/wake.

17.Huduma za wagonjwa majumbani zinatolewa.

18.Timu ya tiba shufaa inawaona wagonjwa wa mawodini kila siku (service word round) na siku ya jumatano ni (major wadi round) kwa floor zote na kwa timu nzima, na siku ya ijumaa ni siku ya kufanya kikao cha timu na kuona changamoto tulizokutana nazo kwa wiki nzima na kupeana mikakati, pia tunafanya mikutano ya familia na kujaribu kutatua matatizo yao.

19.Tunapokea wanafunzi na watoa huduma za afya kutoka sehemu mbali mbali wanaokuja kwa ajili ya mafunzo ya Tiba Shufaa na matumizi bora ya dawa ya Morphine.

20.Kila huduma inayotolewa kwenye kitengo inarekodiwa na kuripotiwa kila mwezi.